

## Mad Ice "Baby Gal"

Visit "[Baby Gal](#)" on MotoLyrics.com

(Chorus)

Kila kitu nachofanya unaona hakifai baby gal, mimi  
nifanyeje?  
Nimefanya mambo mengi nikuridhishe wee lakini gal,  
You driving me crazy.  
Nifanye kitu gani uelewe!  
Nifanye jambo gani uridhike!  
... Baby gal... (rough voc)

(Verse 1)

Nilihitaji unionyeshe mapenzi, Ooh ulinionyesha.  
Sikuhitaji unifanyie upuuzi, Ooh ungenikondesha.  
Nilikupa chochote ulichotaka, mradi nisione  
unahangaika.  
Lakini bado ulinifanyia pupa, tamaa kichwani  
zilikuzunguka.  
Nilihisi labda umenichoka, kumbe tamaa tu  
zinakuhangaisha.  
Nionyeshe mapenzi na huba, hivyo vyote mpenzi  
vinapita x2

(Chorus x2)

(Verse 2)

Ulimtamani mwenye simu mkononi, Ooh nami  
nikanunua.  
Ulimtamani mwenye dreads kichwani, Ooh kama  
nywele nikafuga.  
Ulinifanya nisifiwe njiani, eti kwa kuwa mii najithamini.  
Ila ukweli wangu upo moyoni, upendo wangu kwako  
niliuamini.  
Kama gari, fedha, nyumba nilikupa.  
Lakini bado penzi letu liliyumba.  
Ulitamani vingine vilivyo bomba, Oh uwo uwo navyo  
ulipata.

(Chorus x2)

(Bridge)

Napenda kukuona ukifurahi lakini jua tamaa haifai.  
Sasa nataka, unieleze unachotaka.  
Sio unione, mimi kama takataka.

Kila nachofanya, kukiona kama taka.  
Utani force. kamba yetu kuikata.  
Wakati muda, bado haujawadia.  
Baby gal baby gal, Hey iyeah iyeah.

(Chorus x2)  
END!

Visit [Mad Ice](#) page on MotoLyrics.com, to get more lyrics and videos.

---

[MotoLyrics.com](#) | Lyrics, music videos, artist biographies, releases and more.